



CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI KITUO CHA MAFUNZO KANDA YA ZIWA-MWANZA

S L P 11957
MWANZA
Tanzania

Simu: +255 28 2560995
Nukushi +255 28 2560994
Barua pepe: mwanza@irdp.ac.tz
Tovuti: www.mwanza.irdp.ac.tz

30 MEI 2022

Ndugu:.....

Anuani.....

YAH: BARUA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA ASTASHAHADA YA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI (BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN RURAL DEVELOPMENT PLANNING)

Ninayo furaha kubwa kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kozi tajwa hapo juu kwa muhula wa mwezi Oktoba. Waliochaguliwa wote wanatakiwa kuripoti Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini- Kituo cha Mafunzo Kanda ya Ziwa, Mwanza mnamo Siku ya **JUMANNE** tarehe **18/10/2022**. Tarehe ya mwisho kuripoti ni **JUMAPILI** Tarehe **30/10/2022** baada ya hapo hakuna mwanafunzi atakayesajiliwa.

Unapokuja kuripoti hakikisha umebeba vitu vifuatavyo ni muhimu:-

1. **Vyeti halisi (Original)** vya Elimu (Hati ya matokeo iliyokwisha muda haitapokelewa)
2. Cheti Halisi cha kuzaliwa
3. Kwa sasa **ADA** kwa mwaka ni **TZS 925,000/=**. (Kulipwa kwa awamu NNE)
4. Ada ya Hosteli **TZS 350,000/= (kwa anayehitaji tu)**.
5. Bima ya Afya ya **NHIF TZS 50,400/=** au kadi ya Bima ya NHIF kwa aliyenayo.
6. Gharama za kupimwa Afya na kujaziwa Fomu ya Matibabu **TZS 5,000/=** (italipwa Chuoni)
7. Ada ya **USAJILI TZS 10,000/=**

Usajili utafanyika kwa mwanafunzi aliyekidhi mahitaji /Sifa zilizotajwa hapo juu.

ADA ya masomo italipwa kwa kutumia nambari utakazopatiwa Chuoni kwa mgawanyo ufuatao:

MUHULA	TAREHE	KIASI	NAMBARI ZA MALIPO
MUHULA WA KWANZA	18/10/2022	325,000/=	MALIPO YOTE YAFANYIKE KWA NAMBARI ZA MALIPO UTAKAZOPATIWA CHUONI (CONTROL NUMBER)
	1/12/2022	200,000/=	
MUHULA WA PILI	WAKATI WA USAJILI	400,000/=	


ADA ya Bweni italipwa kwa nambari utakazopatiwa Chuoni kwa awamu zifuatazo:

MUHULA	TAREHE	KIASI	NAMBARI ZA MALIPO
MUHULA WA KWANZA	18/10/2022	175,000/=	MALIPO YOTE YAFANYIKE KWA NAMBARI ZA MALIPO UTAKAZOPATIWA CHUONI (CONTROL NUMBER)
MUHULA WA PILI	WAKATI WA USAJILI	175,000/=	

KUMBUKA: Kabla ya Kufanya Malipo yoyote, hakikisha vyeti vyako vyote ni Halisi. Unataarifiwa kuwa pesa yoyote ikishalipwa Chuoni haitorejeshwa.

Chuo hakina utaratibu wa kutoa Chakula kwa Mwanafunzi bali kuna migahawa ndani na Jirani ya Chuo kwa bei nafuu. Hakuna Sare kwa Wanachuo, wanashauriwa kuvaa nguo za heshima ambazo zinakubalika na kufata miongozo ya Seriakli katika mavazi. Hatua za Kinidhamu zitachukuliwa ikiwepo kufukuzwa Chuo au kusitishwa masomo kwa yeyote atakayekiuka Sheria na Kanuni za Chuo.

Tunategemea kukupokea Chuo cha Mipango-Mwanza kwa kuanza masomo; Karibu sana. Daima tunasema '**Kupanga ni Kuchagua**'



DKT. DANIEL MPETA
MKUU WA TAALUMA

SIMU: 0748002462, 0748 000 648, 0748000649, 0748 002460, 0748002461, 0742 001113